# LEARNING BY EAR 2011

## “The Promised land - A Story of African Migration to Europe”

## EPISODE NINE: “I Do, But Who Are You?”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Katrin Ogunsade, Klaus Dahmann**

**KISUAHELI:Eric Ponda**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: LINDA AND CHARLES AT THE REGISTRY OFFICE**

- **Linda (f, 20)**
- **Florence (f, 35)**
- **Charles (m, 45)**

**SCENE TWO: CHIVASI PAYS LINDA MARAGA'S FAMILY A VISIT**

- **Chivasi (m, 22)**
- **Mr. Maraga (m, 60)**
- **Mrs. Maraga (f, 55)**

**SCENE THREE: CHIVASI CALLS LINDA ON FLORENCE'S MOBILE**

- **Chivasi (m, 22)**
- **Linda (f, 20)**
- **Florence (f, 35)**

**INTRO:**

Hujambo na karibu kwa makala nyingine ya Noa Bongo Jenga Maisha yako. Hii ni sehemu ya tisa katika mfululizo wa mchezo huu “**Ardhi ya ahadi kuhusu Uhamiaji wa Waafrika hadi Ulaya”.** Katika kipindi kilichotangulia mambo yanakwenda kwa kasi kuliko alivyotarajia Linda. Tayari alikuwa na wasiwasi kuhusu tatizo la pesa wakati babake anapompigia simu kumuarifu kwamba yeye na mamake wamefukuzwa kazi. Linda anakukubali pendekezo la rafiki yake Florence kufanya kazi katika klabu ya kuuza pombe usiku. Aidha anaridhia pendekezo la kutafuta cheti bandia cha ndoa. Kwani kwa kufanya hivyo anaamini ataweza kupata kibali cha kufanya kazi na kulipwa mshahara mzuri Ulaya. Lakini Je, Linda anafahamu athari zake? Kwingineko huko Afrika Kaskazini Farahani anatofautiana vikali na rafiki yake Sule baada ya kufuatia kwa ghasia za kisiasa nchini mwao. Je wataridhiana? Au huu ndio mwisho wa urafiki wao? Ungana nasi katika kipindi cha leo. **“Nakubali lakini wewe ni Nani?”** Na tunaanzia ofisi ya sheria ambako Linda anakamilisha utaratibu wa ndoa na kufunga ndoa na mume ambaye hajawahi kumuona maishani mwake katika harusi bandia iliyopangwa na Florence.

**SCENE ONE: LINDA AND CHARLES AT THE REGISTRY OFFICE**

1. **FLORENCE:** **(very excited)** Wow!! Linda, umefaulu! Pongezi kwenu nyote wewe na Charles, na nawatakia maisha mazuri.

2. **LINDA:** **(shortly)** Asante sana!

3. **CHARLES:** Samahani mabibi! Sasa nataka kuondoka. Linda umependeza kweli kama Bi.Harusi! Nadhani Florence amekuarifu kuhusu kila kitu? Mambo unayohitajika kufanya?

4. **LINDA:** Ndiyo, ameniarifu. Kwamba nahitajika kukutembelea nyumbani kwako angalau mara tatu kwa wiki ili kuthibitisha kweli sisi tumeoana mbali na kukulipa kiasi cha Euro 800 kila mwezi.

5. **CHARLES:** Sawa kabisa! Hizi ni funguo za nyumbani kwangu. Tafadhali nipigie simu au unitumie ujumbe wakati unataka kuja. Nakutakia kila la kheri.
6. **FLORENCE:** Kwa hiyo Bi Charles! Unajihisi vipi kama mke wa ndoa. Na mumeo Je?

7. **LINDA:** Florence, kwa hakika nimeudhika sana kwa kitendo hiki kilichotokea sasa hivi. Najihisi msaliti mkubwa maishani mwangu! Yaani sijielewi. Na kwa muda wote wa sherehe sikufahamu kilichokuwa

kikiendelea. Hata wakati nikisema “ndio nakubali” nimekuwa nikijiuliza, na huyu mume ni nani?

8. **NARRATOR:** Linda aliwasili Ulaya, akiwa muoga japo msichana mwerevu, na mwenye heshima zake. Miezi michache baadaye amefunga ndoa na mume ambaye hajawahi kumtia machoni, na kulazimika kufanya kazi saa nyingi katika klabu ya usiku ili aweze kumlipa Charles kwa kumsaidia aweze kupata cheti cha ndoa na stakabadhi za uraia. Wateja wanampenda sana kwenye klabu hiyo na anapata pesa nyingi kama bakshishi. Lakini tukirejea nyumbani, Chivasi hajazungumza na Linda kwa muda sasa na ameanza kuingiwa na wasiwasi. Ili kutuliza moyo wake, anaamua kumtafuta Linda. Na watu wanaoweza kumsaidia ni wazazi wake. Hivyo jioni moja, anaamua kuwatembelea wazazi wa Linda.

**<u>SCENE TWO: CHIVASI PAYS LINDA MARAGA'S FAMILY A VISIT</u>**

9. **SFX: DOG BARKING LOUDLY**

10. **MR. MARAGA:** Mama Linda, hebu tazama nani anabisha mlangoni? Kwani huyu Mbwa ameanza kupatwa kichaa. Akiendelea kubweka namna hii nitampeleka kituo cha matibabu ya mbwa!

11. **MRS. MARAGA:** Oh, Mume wangu! Nadhani unayosema ni mzaha tu?

12. **SFX: METAL DOOR BEING UNLOCKED**

13. **MRS. MARAGA:** **(pleased)** Oh..! ni wewe, Chivasi? Pita ndani! Umetoweka tangu Linda asafiri kwenda Ulaya.

14. **CHIVASI:** **(nervously)** Samahani sana kwa kuwatembelea wakati wa usiku na kisha bila ya taarifa. Sitachukua muda mwingi. Nataka tu kuwauliza.-

15. **MRS. MARAGA:** Basi pita ndani!. Na uwache kujifanya mgeni hapa! Hapa ni nyumbani kwako! Pita ndani! Kwani hujui Waafrika wanaamini kuwa mgeni ni malaika na huleta baraka?

16. **CHIVASI:** Sawa!… Ni sawa. Asante sana Mama Maraga! Lakini sitakawia.

17. **SFX: METAL DOOR LOCKED**

18. **MR. MARAGA:** Chivasi, mtoto wangu! Karibu sana! Habari za siku nyingi? Mbona unaonekana na wasiwasi? Kwani kuna tatizo?

19. **CHIVASI:** Ni Linda! Hatujawasiliana naye kwa muda wa miezi kadhaa sasa. Na si kawaida yake kabisa! Wakati alipowasili Ulaya mara ya kwanza tulikuwa tukiwasiliana mara kwa mara. Lakini sasa amekata mawasiliano. Ndiyo sababu ya kuja kujua ikiwa mmewasiliana naye hivi karibuni.

20. **MRS. MARAGA:** **(excuses herself)** Samahani nitawaacha muendelee na mazungumzo. Niko jikoni nawatengezea chai. Chivasi nikutengenezee kikombe cha Chai?

21. **CHIVASI:** Asante sana, mama, Maraga! Kama nilivyotangulia kusema nisingependa kukawia.

22. **MR. MARAGA:** Eeee… Umesema bado hujawasiliana na Linda kwa zaidi ya miezi miwili?

23. **CHIVASI:** Miezi miwili, siku tisa… na saa 18 kwa uhakika. Je anaendeleaje?

24. **MR. MARAGA:** Anaendelea vizuri. Pengine anahitaji muda zaidi kujipanga na masomo kwanza.

25. **CHIVASI:** Mzee Maraga, namjua vizuri sana Linda. Hawezi kunifanyia mimi hivi…. pengine... **(swallows hard)** …pengine amepata mwingine huko Ulaya.

26. **MR. MARAGA:** **(comforting)** Hapana, hapana! Usiseme hivyo, Chivasi! Linda anakupenda sana! Na isitoshe – kama angekuwa amepata mwingine, tungekuwa wa kwanza kufahamishwa. Yeye hatufichi chochote! Nimezunguma naye wiki moja iliyopita. Na sidhani kama amebadilika.

27. **CHIVASI:** Unaweza kunisaidia namba yake. Nitajaribu

kumpigia? Nahitaji sana kuzungumza naye.

28. **MR. MARAGA:** Lakini si nambari yake, ni ya rafiki yake! Anaitwa Florence. Nafikiri wanasoma pamoja, lakini sijamuuliza!

29. **CHIVASI:** Tafadhali unaweza kunipa hiyo namba ya Florence?

30. **MR. MARAGA:** Bila shaka! Na utakapozungumza naye tafadhali msalimie sana! Hebu subiri kidogo. Hiyo namba iko kwa simu yangu.

31. **SFX: MOBILE PHONE BOOK BEING BROWSED WITH BEEPING SOUNDS**

32. **MR. MARAGA:** Ah – Sawa hii hapa. Una kalamu na karatasi….uiandike?

33. **CHIVASI:** Ndiyo.

34. **SFX: PEN SCRIBBLING DOWN ON PAPER**

35. **CHIVASI:** Asante sana. Sasa naomba kuondoka.

36. **MR. MARAGA:** **(shyly)** Eeeh… Chivasi, unakumbuka mke wangu alivyotangulia kusema? Kwamba wageni huleta baraka…? Ukweli ni … ukweli ni kwamba,.. kwa wakati huu familia hii inapitia kipindi kigumu sana

kifedha. Nilikuwa…naomba kama una uwezo wa kutusaidia na kiasi cha pesa kidogo? Kwa muda tu. Nadhani unatuelewa!

**37. CHIVASI:** **(concerned)** Bila shaka. Poleni sana kwa yote mnayopitia. Linda hajaniambia chochote. Sina pesa nyingi lakini….

**38. SFX: WALLET BEING OPENED; RUSTLING OF BANK NOTES**

**39. CHIVASI:** Nadhani hizi zitamsaidia kwa sasa! Tafadhali nifahamisheni kama mna msaada wowote mnaohitaji kutoka kwangu. Msiwe na wasi wasi wa kunirudishia pesa hizi . Kwaheri Mzee, Maraga.

**40. MR. MARAGA:** **(overjoyed)** Ohh, Chivasi! Asante sana. Mungu akubariki sana mwanangu. Kwaheri!

**41. NARRATOR:** Chivasi hajaamini aliyoambiawa na Mzee Maraga. Kwamba Linda amezungumza nao hivi punde na asizungumze naye. Lakini kinachomsikitisha zaidi ni habari za kuachishwa kazi na matatizo ya kifedha yanayoikumba familia ya Mzee Maraga. Na Jambo linalomshangaza zaidi ni kwamba Linda hajamzungumia chochote kuhusina na hilo. Baada ya kuondoka nyumbani kwao anaenda moja kwa moja hadi kwenye kibanda cha huduma nafuu, kupiga simu ya kimataifa. Ni usiku huko Ulaya na Linda ameingia zamu yake ya usiku kazini. Florence pia yuko katika klabu hiyo akipata kinywaji.

**SCENE THREE: CHIVASI CALLS LINDA ON FLORENCE'S MOBILE**

42. **SFX: BACKGROUND TECHNO MUSIC PLAYING**

43. **SFX: MOBILE PHONE RINGING**

44. **FLORENCE:** **(bit tipsy)** Hello, nani mwenzangu?

45. **CHIVASI:** Hello, Florence? Naitwa Chivasi. Mimi ni mchumba wake Linda. Nimepewa namba yako na babake Linda. Ameniambia kwamba wewe ni rafiki mkubwa wa Linda chuoni…? Yuko karibu? Tafadhali naweza kuongea naye?

46. **FLORENCE:** Chivasi? …Ah ndiyo bila shaka. Wewe ndiye Chivasi. Sikiliza -Ana shughuli nyingi sana kwa sasa.

47. **CHIVASI:** Na huo ni muziki wa nini nausikia kwa mbali? Ana shughuli nyingi akifanya nini mpaka hawezi kuzungumza na mimi, japo kwa dakika moja tu?

48. **FLORENCE:** Kwanini unaniuliza maswali mengi! Sipendi tabia ya aina hiyo. Kwanza kwa taarifa yako sahau kabisa mambo ya Linda? Tafuta msichana mwingine umuoe.

49. **CHIVASI:** **(utterly shocked)** Eti nini ?! Una thubutu kuniambia

mimi hivyo? Sikiliza hapa Florence, sijui unaitwa nani: Mimi na Linda ni wachumba na tunatarajia kuoana hivi karibuni, upende usipende!

**50. FLORENCE:** Oh, kweli? sawa – wacha nikupe uzungumze naye. Endelea kuota hiyo ndoto! **(shouts)** Wewe! Lindaaa… Chivasi yuko kwa laini ya simu.

**51. LINDA:** **(surprised - in a low voice, so Chivasi doesn’t hear)** Chivasi? Alipata wapi namba yako ya simu… lazima alipewa na babangu **(urgently)** mwambie siko!

**52. FLORENCE:** **(also in a low voice, humouring her)l** Tayari nimemwambia. Lakini anasisitiza kwamba hivi karibu mtafunga ndoa. Hana habari kwamba tayari umeolewa. **(laughs)**

**53. LINDA:** **(low voice)** Tafadhali Florence, kata hiyo simu – siko tayari kuongea naye sasa.

**54. FLORENCE:** **(low voice)** Sawa – utakavyo Bi Charles.

**55. SFX: BEEP OF MOBILE PHONE CALL DISCONNECTING**

**56. LINDA:** Florence, Nafikiri bora nirudi nyumbani. Nimepata pesa za kutosha kugharamia nauli ya kunirejesha nyumbani. Natamani sana kuwaona wazazi wangu.

Pia nahitaji kupumzika.

**57. FLORENCE:** Ni sawa. Lakini kwanza umlipe Charles pesa zake kabla ya kuondoka. Na unaweza kwenda kwa muda wa wiki moja tu. Ni sawa?

**58. LINDA:** Sawa. Nimesikia!

**OUTRO:**

Na huku Linda anaporejea kazini kwa zamu ya usiku kuwahudumia wazungu walevi katika klabu hiyo ndipo tunafika mwisho wa sehemu hii ya tisa. Linda anaamua kurudi nyumbani kupumzika kwa muda wa wiki moja. Je mambo yatakuwaje wakati atakapokutana tena na wazazi wake na mchumba wake Chivasi? hasa baada ya Florence kumweleza Chivasi asahau kabisa mambo ya Linda? Je atafanya nini kudumisha uchumba huu na mpenzi wake wa tangu utotoni? Na je, kuhusu rafiki yetu Farahani kutoka Afrika Kaskazini. Unamkumbuka? Huku nchi yake ikiwa imetumbukia kwenye ghasia, je bado ana mipango ya kujaribu tena kuhamia Ulaya kinyume cha sheria? Kwa haya, na mengine mengi ungana nasi tena kwa kipindi kinachofuata. Na ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki usisite kutembelea mtandao wetu wa dw.de/destinationeurope. Hadi wakati mwingine kwaheri kwa sasa.